USALAMA WA CHAKULA

# TMB yateketeza kilo 171 za nyama

Habel Chidawali, Mwananchi
hchidawali@mwananchi.co.tz

**Dodoma.** Kilo 171 za nyama ya ng'ombe zenye thamani ya Sh1.2 milioni zimeteketezwa na Bodi ya Nyama Tanzania (TMB) kwa kuingizwa sokoni bila kukaguliwa.

TMB pia imemtoza faini ya Sh300,000 Elisha Daudi kwa kosa la kuuza bidhaa hiyo bila kukaguliwa na wataalamu na kuisafirisha kwa kutumia pikipiki hali inayotajwa kuhatarisha afya za walaji.

Ofisa Mifugo wa TMB, Alex Mkenda alisema sababu ya kuteketezwa kwa nyama hiyo ni kutokana na baadhi ya mifugo kutokaguliwa kabla ya kuchinjwa au kuandaliwa katika machinjio yasiyosajiliwa na TMB ambayo kisheria ndiyo yanaruhusiwa kufanya hivyo kwa ajili ya afya ya watu.

Mkenda alitaja sababu nyingine kuwa ni ubebaji wa nyama hiyo kwa kutumia pikipikiki kinyume na sheria ya ubebaji wa kitoweo hicho inayoelekeza yatumike magari maalumu yaliyosajiliwa na TMB.

"Usafirishaji wa nyama unapaswa kufanywa kwa kutumia magari maalumu (meat van), yaliyokaguliwa na kusajiliwa na Bodi ya Nyama Tanzania kwa lengo la kuhakikisha usalama wa nyama unazingatiwa," alisema.

Ofisa Mifugo wa Kata ya Viwandani, Elia Mtamwa alisema wafanyabiashara wa nyama wamekuwa wakifanya mambo hayo kwa makusudi kwani mara kadhaa wamepewa elimu lakini hawataki kuzingatia wala kufuata.

Mtamwa alisema kutofuata sheria mara nyingi kunasababisha matukio ya wizi wa mifugo ambayo inachinjwa kiholela na kuuzwa buchani bila kukaguliwa na wataalamu wa nyama.

Hata hivyo, ofisa huyo alitaja ugumu wa mapambano dhidi ya wafanyabiashara hao akisema ni "zaidi ya vita vya dawa za kulevya kutokana na biashara kufanyika usiku huku nyama ikiwa imefungashwa kwenye mifuko isiyo salama."



**'Usafirishaji wa nyama unapaswa kufanywa kwa kutumia magari maalumu yaliyokaguliwa na kusajiliwa.'**

Alex Mkenda, ofisa TMB.

Mfanyabiashara aliyekamatwa na nyama hiyo, Elisha Daudi alikiri kukutwa na bidhaa hiyo na kuahidi kutorudia tena kutenda makosa hayo ambayo yamekuwa yakifanyika kwa mazoea hata na wafanyabiashara wenzake.

Daud alisema Sheria Nyama namba 10 ya mwaka 2006 na kanuni zake zinaelezea namna Bodi ya Nyama Tanzania inavyopaswa kusimamia tasnia ya nyama na usalama kuzingatiwa ikiwamo kutumia machinjio rasmi yaliyoidhinishwa na kuridhiwa na bodi.

Kwa sasa bodi hiyo inaendesha operesheni kwa kushirikiana na wataalam wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi ambapo maeneo mengi wanashtukiza hasa mabucha inakouzwa nyama.

## HIVI NDIVYO TUNAVYOFANYA

Mshauri wa sera wa mradi wa USAID Sera Bora, David Nyange (kushoto) akifafanuliwa jambo na Mkuu wa Uandaaji wa Maudhui wa Mwananchi Communications Limited (MCL), Detricia Pamba alipofanya ziara makao makuu wa MCL jijini Dar es Salaam jana. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa MCL, Bakari Machumu. **Picha na Sunday George**



Kwa upande wa maradhi serikali imepiga hatua kubwa zaidi hasa katika ujenzi wa zahanati, vituo vya afya, hospitali

makubwa.
Katika mpango wa maendeleo baada ya uhuru, serikali

afya, hospitali za wilaya, mkoa, maalumu, kanda na taifa ili kupunguza vifo na maradhi.

sasa hivi ni kukiendeleza kile tulichofanikiwa," anasema Balozi Shimbo.

limeweza kupata ... wake baada ya hatua kubwa ya uwekezaji wa serikali kwenye

Shimbo.
Balozi Shimbo anasisitiza

gane bila kujali ... zetu lakini tunapokuja kuongelea mambo ya maendeleo ya nchi

bima ya afya kwa wote.
Ngole anasema bima ya afya

sha kwa tija.

HABARI LEO UK 12.

# Wazalisha vifaranga nchini na kilio soko la ndani



**Na Mwandishi Wetu**

KATI ya harakati za kuinua uchumi zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dk Samia Suluhu Hassan ni kuiwezesha Tanzania kuendelea kupaa kiuchumi kwa kuifungua nchi na fursa za kiuchumi.

Dk Samia amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha harakati hizi zinazaa matunda na hatimaye kuwawezesha Watanzania kunufaika na ajira kutokana na kuzidi kufunguka kwa fursa.

Sekta ya mifugo hususani ufugaji wa kuku imekuwa ni kati ya sekta ambazo zinachangia ajira kwa vijana hasa kutokana na biashara hiyo kufanyika maeneo mbalimbali ya nchi. Hata hivyo, inagubikwa na changamoto ya uingizwaji wa vifaranga kutoka nje ya nchi.

Upo uhusiano wa karibu kati ya biashara ya uzalishaji wa vifaranga na ufugaji wa kuku na kuwa viwili hivyo vinategemeana kwa ukaribu zaidi hasa ikizingatiwa kuwa kuku anayefugwa anatokana na vifaranga ambavyo kwa hali ilivyo kwa sasa hapa nchini licha ya kuwa na wazalishaji wa vifaranga wa ndani, wapo watu na zipo kampuni ambazo zinaagiza vifaranga kutoka nje.

**Utata wa vifaranga vyenyewe**

Licha ya wazalishaji wa ndani kuwa na uwezo wa kuzalisha kuna njia mbili zinatumika kuagiza vifaranga, moja ni halali nayo ni kupitia kampuni zilizopewa vibali ingawa kampuni za ndani zinapinga vikali vibali hivyo.

Njia ya pili ni kuingizwa kwa njia zisizo sahihi kisheria. Wapo wafanyabiashara wanaingiza vifaranga vya kuku kwa njia za panya na wanakwepa kulipa ushuru.

Kundi linaloingiza kwa njia za panya ni hatari zaidi kwa kuwa licha ya kulikosesha taifa mapato ni mwiba kwa wazalishaji wa ndani wa vifaranga kwa kuwa wao huuza vifaranga kwa bei rahisi tofauti na bei za vifaranga vinavyozalishwa nchini.

Hapa ndipo wazalishaji wa ndani wanapoanza kuona biashara hii ni mwiba kwao kwa kuwa wafugaji wa kuku wanaweza kununua vifaranga hivi vya bei rahisi kwa kuwa wanaona kuwa inawarahisishia biashara zao na kupata faida zaidi.

Vifaranga vya wauzaji walanguzi vinaanzia Sh 1,700 wakati wazalishaji wa ndani wanauza Sh 2,000 kwa kifaranga kimoja. Wazalishaji wa ndani walipoamua kushuka na kuuza kwa Sh 1,800 kwa kifaranga walanguzi waliuza Sh 1,500.

Hali hiyo imekuwa ikisababisha wafugaji kununua vya bei ndogo na matokeo yake vikikua na kufikia muda wa kuuza kuku wauzaji wanauza kwa bei hadi Sh 5,000 na wauzaji wa ndani kuuza kuku Sh 6,200 hali ambayo inawapa ugumu sokoni. Utafiti unaonesha vifaranga vya magendo vingi vinatoka Malawi na Kenya.

**Kauli ya chama cha wafuga kuku**

Mwenyekiti wa Chama cha Wafugaji wa Kuku wa Nyama Tanzania (TABROFA), Aloyce Makoye anasema kama hatua za haraka zisipochukuliwa vifaranga vya nje vinaenda kuua kampuni za ndani za kuzalisha vifaranga.

Anashauri serikali kusitisha vibali kwa kampuni zinazojihusisha na kuingiza vifaranga nchini kutoka nje na kuisihi kuziwezesha kampuni za ndani zikiwepo zile zinazomilikiwa na wawekezaji kutoka nje ya nchi kupata uhakika wa soko.

"Kwa sasa ninaiomba serikali kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kusitisha uagizwaji wa vifaranga kutoka nje ya nchi kuingia hapa nchini, hatua hii italinda masoko ya ndani kama Interchick, Kibo, Organia na Alvin pamoja na wengine ambao kwa sasa wanalalamika biashara ni ngumu, nashauri ufanyike ukaguzi wa kina wa mipaka kuzuia uingizwaji wa vifaranga kiholela," anasema Makoye.

**Mwekezaji wa uzalishaji wa vifaranga anena**

Mkurugenzi wa Kampuni ya Kuzalisha Vifaranga ya Organia, Albert Momdjian ambaye kampuni yake imewekeza zaidi ya Dola za Marekani milioni 30 (Sh bilioni 60) katika uzalishaji wa vifaranga anasema kuwa pamoja na serikali kudhibiti vifaranga vya magendo, bado kuna masoko yanafanya baishara hiyo haramu.

Anasema kuwa kutokana na uingizwaji wa vifaranga hivyo, kampuni yake imeanza kuingia hasara na iwapo changamoto hiyo isipotatuliwa hali inaweza kuwa mbaya.

Mondjian anasema kuwa lengo lake ni kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi inayouza vifaranga ndani na nje ya nchi na kama kukiwa na ushindani wa haki wa uuzwaji wa vifaranga anaweza kujiimarisha kutoka Tanzania na kuanza kuuza vifaranga hadi nchi nyingine za Afrika Mashariki na Kati.

Anasema, wazalishaji wa kuku nchini wana imani kubwa na Serikali ya Rais Dk Samia kuwa itakabiliana na uingizwaji wa vifaranga kutoka nje ya nchi hasa ikizingatiwa kuwa vipo vinavyoingia kwa njia za panya.

Anasema kuwa wazalishaji wa ndani wana uwezo wa kuzalisha vifaranga na kutosheleza soko na kuacha vifaranga vya nje viingie kiholela vinahatarisha usalama wa kuku wa ndani kwa kuwa wanaweza kuleta vyenye magonjwa.

**Serikali yatoa tamko**

Akizungumzia malalamiko hayo Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo ambaye ndiye mtoaji wa vibali vya kuingiza mifugo ikiwemo vifaranga, Profesa Hezron Nonga, anasema kampuni zinazoingiza vifaranga ni mbili ambazo ni Wolowolo Animal Care Center na The One Agro Enterprise ambazo zilipata vibali kuanzia mwaka jana na kwamba vifaranga vinavyoingizwa ni katika kumalizia maombi yao za zamani.

"Hizi kampuni ziliomba vibali katika kipindi ambacho nchi ilikuwa na changamoto ya uhaba wa vifaranga ambapo The One Agro Enterprise imeruhusiwa kuingiza vifanga 494,000 kutoka Uganda na Wolowolo vifaranga 150,000 kutoka Malawi na mwisho wakuingiza ni Januari 15, 2023," anasema Profesa Nonga.

Aidha, anasema kushuka kwa bei ya kuku katika soko kunatokana na kipindi husika na hali ya uchumi na kwamba matarajio yao ni kuanzia Desemba biashara itakuwa nzuri zaidi.

Lakini ameahidi kufuatilia watu wanaoingiza vifaranga kwa njia za panya na kuhakikisha wanachukuliwa hatua kulinda wazalishaji wa ndani.

**Muuza kuku azungumzia kadhia**

Mwanahawa Manyama wa Gongo la Mboto anasema kuwa kwa wafugaji kama yeye ambao wananunua vifaranga vya wazalishaji wa ndani huuza kwa Sh 6,400 kwa kuku mmoja lakini kutokana na uwezo wa wauzaji wa kuku kutoka kwenye vifaranga vya magendo wanaouza hadi Sh 5,700 na wao hulazimika kushusha bei kwa kuwa wanakosa wateja.

Anasema: "Yaani kama hakuna hatua za kudhibiti vifaranga vya magendo basi wafugaji wote tutajikuta tunakimbia kununua vifaranga kwa wazalishaji wa ndani ambao ndio wanalipa kodi na kwenda kununua hivi vya magendo sasa hapo kunakuwa na shida.

"Lakini ni imani yangu kuwa Rais Samia ana macho na changamoto hii itatatuliwa."

CamScanner

kura alizopigiwa Rais wa Zanzibar
yekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.
Ali Mwinyi na Wajumbe wa Mkutano
10 wa Chama Cha Mapinduzi (CCM),
kamu Mwenyekiti wa CCM, Zanzibar.
pigwa zilikuwa 1,915

UHURU UK 1

# Nyama ya ng'ombe yateketezwa



BODI ya Nyama Tanzania (TMB), imeteketeza kilo 171 za nyama ya ng'ombe yenye thamani ya sh. milioni 1.2 na kumtoza mfanyabiashara faini ya sh. 300,000...

Habari Uk. 9

# Hospitali ya sh.bilioni 12 kuanza huduma

Habari Uk. 3





WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Dk. Stergomena Tax, akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje wa Oman, Sayyid Badr Al Busaidi, wakati wa Mkutano wa Pili wa Tume ya Kudumu ya Pamoja ya Ushirikiano (JPC) kati ya Tanzania na Oman, jijini Muscat, mwishoni mwa wiki.

UHURU UK 8

# Wazalishaji bidhaa za ngozi watamani soko nje ya nchi

NA GIFT MONGI, *Moshi*

WAZALISHAJI wa bidhaa za ngozi nchini wamesema licha ya serikali kuondoa tozo katika bidhaa hizo, kuna umuhimu wa kutafuta masoko ya uhakika nje ya nchi yawasaidie kunufaika zaidi.

Mkurugenzi wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Woisso Original Products (WOP), Kenneth Woisso alisema serikali imeweka jitihada mbalimbali katika kukuza soko la ngozi, lakini ipo haja ya kutafuta masoko ya uhakika biashara hiyo ikue zaidi.

Alisema kuuza bidhaa hizo kwa mteja mmoja bila kuwa na uhakika wa soko bado vigumu kupata manufaa makubwa, lakini kama zitatumika njia nyingine mfano ubalozi wa Tanzania kuunganisha wanunuzi na wazalishaji wa ndani anaamini biashara hiyo itaimarika zaidi.

Kwa mujibu wa mkurugenzi huyo, China ina mtaji mkubwa, hivyo ni vyema wazalishaji wa ndani wakajipanga kutosheleza soko la uhitaji kukidhi mahitaji ya kila siku.

"Wenzetu (China) wanajiweza kimtaji hivyo na sisi kama tunaenda kufanya nao biashara ni lazima tujipange kikamilifu maana kwanza hatuna uzoefu, lakini hata mteja mwenyewe hatujui kwa kumpata," alisema.

Woisso alisema bado ipo haja serikali kuendelea kuwashika mkono wadau wa sekta ya ngozi kwa kuwatafutia mtandao wa masoko ya nje kwa sababu bado sekta hiyo haijaanza kufanya vizuri.

Alibainisha kama biashara hiyo itakua na kufanya vizuri kama ilivyo dhamira ya serikali, wafugaji nao watanufaika kwani malighafi inayotokana na mifugo itakuwa na soko la uhakika.

Kwa upande wake, Kelvin Msaki ambaye ni muuzaji wa ngozi alisema hivi sasa biashara hiyo imeonekana kukumbukwa tofauti na ilivyokuwa huko nyuma ambapo jitihada hizo zikiendelea sekta hiyo itaenda kufikia mahali pazuri.

**Ipo HAJA**

Serikali kuendelea kuwashika mkono wadau wa sekta ya ngozi kwa kuwatafutia mtandao wa masoko ya nje kwa sababu bado sekta hiyo haijaanza kufanya vizuri.